**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**

**Shule ya Sekondari Kiwanja**

**S.L.P. 178,**

**CHUNYA.**

**Kumb. KJSS/JI/2025/02**

**Tarehe ………..**

Mkuu wa shule: 0754 603 777
Makamu Mkuu wa shule : 0764663566
Patron/Matron: 0752518470 /0768106598
Mwandamizi taaluma 0763517911
Mwandamizi malezi 0768717368

Mzazi/ Mlezi wa ____________________
S.L.P. ____________________________
___________________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI KIWANJA ………..**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano katika shule ya Sekondari Kiwanja kuanzia mwezi ………. katika tahasusi ya **CBG, HGK, HKL, HGL, HGE, PCB, HGLi, HGFa (kata isiyo husika).** Shule ya Sekondari Kiwanja ipo umbali wa Kilometa **70** kutoka Mbeya mjini.

Usafiri wa basi unapatikana katika kituo cha mabasi Mbeya mjini (Uwanja wa ndege wa zamani) na nauli mpaka chunya ni shilingi Tshs. **4000/=** Unaweza kuwaomba kushukia shuleni kabla ya kufika Chunya mjini au unaweza kushukia chunya Mjini na kuja Shuleni kwa Bodaboda kwa Tshs 1,000/= **(kamwe mwanafunzi asisafiri na simu, mzazi unashauriwa kuwa na mwasiliano na wenye mabasi kujua kama mwanao amefika na mara afikapo shuleni atakupigia simu kwa namba 0752518470. Kama huamini kuwa atafika peke yake ni afadhari umlete wewe mwenyewe)**

Muhula wa masomo unaanza tarehe **..........** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **..............** kwa ajili ya kuanza masomo tarehe **..............** Mwisho wa kuripoti ni tarehe
**...................**

## 2. MICHANGO MBALIMBALI.

Kila mzazi anatakiwa kumlipia mwanae michango ifuatayo:

| S/N | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Michango ya uendeshaji shule | **65,000** |
| 2 | Tahadhari | **5,000** |
| 3 | Nembo | **5,000** |
| 4 | Kitambulisho | **5,000** |
| | **JUMLA** | **80,000** |

Jumla ya fedha **Tshs 80,000/=** zilipwe kwenye Akaunti ya shule Namba. **60706600128** katika Benki ya NMB Jina la akaunti ni **KIWANJA SECONDARY SCHOOL (tafadhali andika jina Ia mwanafunzi kwenye pay in slip)**. **Hatupokei fedha taslimu kabisa shuleni tafadhali lipa benki na uje na karatasi halisi (Original) ya hati ya malipo (bank slip).**

## 3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

### 3.1. SARE YA SHULE

a. Suruali/siketi 2 rangi ya ugoro. Maelezo ya mshono wa suruali mifuko iwe ya kawaida (**mifuko ya mfumo wa suruali ya jinsi haikubaliki**), isiwe nyembamba iwe pana miguuni. Sketi iwe ndefu inayofika kwenye kisigino cha mguu mshono ni linda boksi ya masisita

b. Mashati meupe ya mikono mirefu mawili kwa wote .

c. Rangi ya Hijabu (kijuba) nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

d. Sare za michezoTrack suit rangi ya bluu kwa wavulana na rangi Nyeusi kwa wasichana, bukta kwa wavulana na raba nyeusi kwa wote.

e. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi jozi 2 kwa wote.

f. Soksi jozi mbili rangi nyeusi kwa wavulana na rangi nyeupe kwa wasichana **.**

g. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.

h. Sweta 2 rangi ya ugoro kwa wote
.

i. Nguo za kushindia (shamba dress) suruali 2 kwa wavulana na siketi 1 kwa wasichana (rangi ya kaki-kitambaa cha pamba) siketi iwe ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu kwa wasichana pia kuna sare ya gauni moja refu mpaka kwenye kifundo cha mguu rangi ya dark blue (aina ya mshono ni solo).
j. Tai mbili kwa wavulana na sikafu mbili kwa wasichana rangi ya ugoro kwa wote.
k. Tisheti mbili (2) rangi ya dark blue zenye kola
l. Mashuka mawili rangi ya light blue kwa wavulana na rangi ya pinki kwa wasichana.

### 3.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni

**i.** Madaftari makubwa kumi (counter book)
**ii.** Ream moja (A4) ya karatasi kwa kila muhula.
**iii.** Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
**iv.** Dissecting Kit, tray na koti nyeupe la maabara la kuvaa wakati wa mazoezi ya vitendo kwa wanafunzi wanaosoma Biology, chemistry na physics.
**v.** Scientific Calculator kwa wanafunzi wa sayansi
**vi.** Godoro ft 2.5.
**vii.** Blanketi 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
**viii.** Nguo za ndani za kutosha
**ix.** Vyombo vya chakula (sahani, bakuli na kikombe)
**x.** Ndoo 2 ndogoo (lita kumi) zenye mifuniko na sabuni lita 01.
**xi.** Kwanja 1, jembe 1, mopa 1, mifagio 2 wa ndani na nje, soft bloom, hard bloom.
**xii.** Aje na kadi yake ya bima ya afya au lipa **Tshs 50,400/-** bank kwa ajili ya bima kama hana bima ya serikali.

## 4. Sheria na kanuni muhimu za shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na:

### 4.1. Sheria na kanuni za shule

i. Heshima kwa viongozi wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhuria mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (preparation)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenyencha kali na dawa bila idhini ya daktari
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa mkuu wa shule (msiba au ugonjwa).**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atumiwe pesa zake za matumizi kwa njia ya wakala wa Bank ya NMB. Mwl. Kasanda na huduma ya lipa kwa M-PESA aliyopo shuleni na siyo sehemu nyingine yoyote kwa mawasiliano ya wakala huyo ni 0768006724.**

## 4.2. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi .
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Kusababisha mimba.
xiv. Kwenda kwenye majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xviii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

**5. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika

mgomo, fujo na makosa ya jinai imeambatanishwa.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, na maelekezo mengine atakayotolewa na shule imeambatanishwa.

d) Picha ndogo moja ya mwanafunzi na passport moja moja za watu wanne(4) Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu,

e) Anatakiwa kuja na cheti cha kuzaliwa pamoja na cheti cha kumaliza kidato cha nne (Leaving certificate) na result slip.

Aje na **faili** moja kwa ajili ya kutunzia nyaraka zake mbalimbali.

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni

mgonjwa na yuko mahututi hivyo atume pesa. **TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

***Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

**KARIBU SANA KIWANJA EKONDARI**

**ELLY J.**
**MNYALAPE Mkuu**
**wa Shule**
**0754 603**
**777**

**OFISI YA WAZIRI MKUU,**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**

**FOMU YA KUKUBALI**

1. Mimi ………………………………………………………………………., nimekubali kuingia kidato cha tano Katika shule ya sekondari kiwanja kama mwanafunzi wa bweni tarehe ………………………… nitafika shuleni bila kuchelewa na kusoma kwa bidii.
2. Nitatii sheria za shule, sitajihusisha wala kuchochea mgomo shuleni. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo, nidhamu na kazi za kujitegemea.
3. Sahihi ya mwanafunzi ………………………………………. Tarehe …………………….

**SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI**

1. Mimi ……………………………………………. Nimekubali mtoto wangu ………………………………… Asome katika shule ya sekondari Kiwanja kuanzia ……………………………………………………….
2. Ninaahidi kumpa vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua.
3. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea.
4. Ninakubali mtoto wangu asome katika shule ya sekondari Kiwanja kama mwanafunzi wa bweni na ataendelea hivyo hadi atakapo maliza kidato cha sita. Naelewa nafasi za bweni ni chache sana, hivyo mimi wala mwanangu hatutamsumbua Mkuu wa shule wala uongozi wa shule kwa vyovyote
5. Anwani yangu ya kudumu ni:

   ……………………………………………

   ……………………………………………

   Sahihi …………………………………… Tarehe…………………………

   Fomu hii inatakiwa kujazwa na ndugu 3 wa karibu wa mwanafunzi:

| **Jina la ndugu** | **uhusiano** | **Mahali anakoishi** | **Namba ya simu** | **Kazi yake** |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINSTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.**

KIWANJA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 178
**CHUNYA**

**TO MEDICAL OFFICER,**

……………………………… **Date: …………….**
………………………………
………………………………

**PART A**

**Student's name** ...........................................................................................

Please examine the above named student to his/her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following:

1. Hemoglobin...........................................................
2. P.V. Bleeding...........................................................
3. Sight...........................................................................
4. Blood pressure.........................................................
5. Urine for sugar and pregnant test...........................
6. Stool for routine examination.................................
7. Asthma.......................................................................
8. Skin diseases..............................................................
9. Leprosy.......................................................................
10. Any deformity............................................................
11. Epilepsy......................................................................
12. Pulmonary tuberculosis..........................................
13. Neurosis......................................................................
14. General diseases..........................................................

**PART B:**

**MEDICAL CERTIFICATE**
**(To be completed by a Government medical Officer)**

I have examined the above named student and consider that he/she is physically and mental **fit/unfit** to join the school for the **year …………**

**………………………………**
**Signature (Dr)**